

MKATE WA SIKU

NENO LA SIKU

Machi 2022

31
SIKU

SIKU 01 – ISAYA 25:1a (SUV)

"Ee Bwana, wewe ni Mungu wangu; nitakutukua; Nitalisifu jina lako, kwa maana umefanya mambo ya ajabu"

SIKU 02 – YEREMIA 31:34b (ESV)

"...maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena."

SIKU 03 – WAEFESO 4:6 (NHN)

"kuna Mungu mmoja na Baba wa wote, ambaye yuko juu ya wote, afanya kazi katika yote na yuko katika yote."

SIKU 04 – ZABURI 139:14b (SUV)

"...Matendo yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana."

SIKU 05 – MAOMBOLEZO 3:26 (BHN)

"Ni vema mtu kungojea kwa saburi ukombozi utokao kwa Mwenyezi-Mungu."

SIKU 06 – WAEBRANIA 13:8 (SUV)

"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele."

SIKU 07 – ISAYA 28:21b (BHN)

"...Atatekeleza mpango wake wa ajabu; atatenda kazi yake ya kustaajabisha."

SIKU 08 – ZAKARIA 10:12 (SUV)

"Nami nitawatia nguvu katika BWANA; nao watatembea huko na huko katika jina lake, asema BWANA."

SIKU 09 – ZABURI 30:2 (BHN)

"Ee Mwenyezi-Mungu, Mungu wangu, nilikulilia msaada, nawe ukaniponya."

SIKU 10 – MATHAYO 6:33 (SUV)

"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa."

SIKU 11 – YEREMIA 32:17 (BHN)

"Ee Mwenyezi-Mungu, ni wewe ambaye kwa nguvu zako nyingi na uwezo wako mkuu, umeziumba mbingu na dunia; hakuna kisichowezekana kwako."

SIKU 12 – YOSHUA 23:14b (SUV)

"...nanyi nyote mnajua mioyoni mwenu, na rohoni mwenu, ya kuwa halikuwapungukia ninyi hata neno moja katika mambo hayo mema yote aliyoyanena BWANA."

SIKU 13 – LUKE 12:7 (BHN)

"Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope, basi; nyinyi mna thamani kuliko shomoro wengi!"

SIKU 14 – ZABURI 107:20a (SUV)

"Hulituma neno lake, huwaponya..."

SIKU 15 – MATHAYO 5:16b (BHN)

"...ni lazima mwanga wenu uangaze mbele ya watu, ili wayaone matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni."

SIKU 16 – ISAYA 60:18 (SUV)

"Jeuri haitasikiwa tena katika nchi yako, Ukiwa na uharibifu hazitakuwa mipakani mwako; Bali utaziita kuta zako, Wokovu, Na malango yako, Sifa."

SIKU 17 – HESABU 6:26 (BHN)

"Mwenyezi-Mungu awaoneshe wema wake na kuwapa amani."

- INAENDELEA...

SIKU 18 – 2 NYAKATI 20:21b (SUV)

"...Mshukuruni BWANA; kwa maana fadhili zake ni za milele."

SIKU 19 – ZABURI 107:29 (BHN)

"Aliifanya ile dhoruba kali itulie, nayo mawimbi yakanyamaza."

SIKU 20 – YOHANA 1:5 (SUV)

"Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza."

SIKU 21 – YOSHUA 2:11b (BHN)

"...Mwenyezi-Mungu, Mungu wenu, ndiye Mungu juu mbinguni na chini duniani!"

SIKU 22 – HESABU 23:21b (SUV)

"BWANA, Mungu wake, yu pamoja naye, Na sauti kuu ya mfalme i katikati yao."

SIKU 23 – MATHAYO 19:26b (BHN)

"Kwa binadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote huwezekana."

DAY 24 – ZABURI 56:4a (SUV)

"Kwa msaada wa MUNGU nitalisifu neno lake. Nimemtumaini Mungu, sitaogopa;"

SIKU 25 – ZAKARI 13:9b (BHN)

"...Hapo wao wataniomba mimi, nami nitawajibu. Nitasema, 'Hawa ni watu wangu', nao watasema, 'Mwenyezi-Mungu, ndiye Mungu wetu.'"

SIKU 26 – YOHANA 15:7 (SUV)

"Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. "

SIKU 27 – YOELI 2:27b (BHN)

"...Mimi Mwenyezi-Mungu, ndimi Mungu wenu wala hakuna mwingine. Watu wangu, kamwe hawatadharauliwa tena."

SIKU 28 – HESABU 14:17 (SUV)

"Basi sasa nakusihi sana, uweza wa Bwana wangu na uwe mkuu, kama ulivyonena, uliposema, "

SIKU 29 – WAFILIPU 4:8b (BHN)

"...Zingatieni mambo mema na yanayostahili kusifiwa; mambo ya kweli na bora; mambo ya haki, safi, ya kupendeza na ya heshima."

SIKU 30 – LUKA 18:27 (SUV)

"Akasema, Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu."

SIKU 31 – MITHALI 3:5&6 (BHN)

"Mtumaini Mwenyezi Mungu kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili ako mwenyewe. Mtambue Mungu katika kila ufanyalo, naye ata inyosha njia yako. "

**Makala hii imechukuliwa
kutoka**

**www.biblesociety.ca © Haki
zote zimeifadhiwa.**

*Tunawashukuru sana kwa
kuungana na sisi kueneza Neno la
Mungu hapa Tanzania na duniani
kote kwa ujumla.*

Chama cha Biblia cha Tanzania

16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>



&



**Canadian
Bible Society**

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA